Umomoni

Na

Ellis p. Forsman

(Mormonism)

Oktober 7, 2011

Umomoni

1 Yohana 4:1

Miaka kadhaa iliyopita, tulikuwa na familia ya vijana waliokuwa wanaishi nasi ambao walikuwa na desturi na milaa ngeni. Gary na Pam walikuwa Wamomoni. Wakati Pam akiwa safifi na dini ya Momoni, Gari alikuwa na shida sana na dini, basi tukaliongelea. Wamomoni wanatazamwa kama watu wema na wa ajabu, lakini kuna baadhi yao wana shida kubwa kuhusu dini yao.

Matangazo ya TVyanawakaribisha watu kujifunza mafundisho ya Kristo kutoka kwa Wamomoni, wanaojiita wenyewe Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Nyakati za Mwisho (Hakuna kitu kama Kanisa la Kristo). Umomoni unachukua uzito mkubwa juu ya neno Mkristo, na kudai kutumia Biblia pamoja na Kitabu cha Momoni, lakini kwa hualisia, wanafahamu kidogo kuhusu Biblia. Kulipo na mkangaanyiko kati yaa vitabu viwili, wanakubali Kitabu cha Momoni kama ndio lenye ukweli. Tutazungumzia hilo badae.

Kwa sababu Wamomoni wanaegemea dini yao sana katika kitabu kinachoitwa Kitabu cha Momoni, ni muhimu kwamba tukaangalia chanzo chake, na kuhakikisha ukweli wake.

Kitabu hiki kiliandikwa na Joseph Smith mwaka 1830, aliyejiita mwenye “Nabii, mtabiri, na Mvumbuzi wa Mungu.” Anadai kuwa alitafsiri kutoka katika maandishi ya kwenye sahani za dhahabu ambazo zilionyeshwa kwake na malaika wa Mungu. Kama kitabu hiki kina ukweli, basi tunapaswa kukifuata, na kama kina uongo, basi inapaswa tuachane nacho.

Kuna uthibitisho mwingi unaoonyesha kwamba Joseph Smith alikuwa nabii wa uongo, lakini Wamomoni hawataukubali ukweli huo. Kwa ushahidi wa kibiblia ambao unapingana na elimu ya dini ya Momoni, hadi katika kupingana na historia yake yenyewe na mafundisho, uthibitisho unafunga. Lakini Wamomoni wanajiweka wakifu kwa dini yao na ushahidi wao, huwezi na hutaona uthibitisho. Hawaegemei katika uthibitisho wa biblia, siyo katika ushahidi wa

kihistoria, bali wanaamini “ushahidi” kwamba Umomoni ni kanisa lililotokana na kanisa na Joseph Smith ni nabii wake wa kweli.

Moja ya majaribio yanayoonyesha kwamba imani iko kwenye msingi wa ukweli ni aidha inaweza kuthibitishwa au haiwezi kuthibitishwa kuwa kweli au siyo kweli. Kama mtu atasema, “Sijali ni uthibitisho gani utanionyesha, nitaamini kila mara,” basi imani ya mtu huyo haijajengwa kwenye ukweli. Na kwa vile Ukristo ni dini ya historia, usulubishi, ufufuo, na kaburi lililokuwa wazi, n.k., ni dini iliyojegwa kwenye ukweli. Kama inaweza kuthibitishwa pasina shaka kwamba Yesu hakufufuka katika wafu, basi Ukristo ni dini ya uongo. Vilevile, kama itathibitishwa kwamba Joseph Smith alikuwa nabii wa uongo, basi Umomoni ni dini ya uongo. Ilitokea tu kwamba kuna uthibitisho kama huu.

- 1 Yohana 4:1, “*Wapenzi msiamini kila roho, bali zijaribuni hizo roho, kwamba zimetokana na Mungu; kwa sababu manabii wa uongo wengi wametokea duniani.*”
- Mithali 14:12, “*Iko njia ionekanayo kuwa sawa machoni pa mtu, lakini mwisho wake ni njia ya mauti.*”

Historia

Kabla hatujaingia kwenye maandiko, ebu tuangalie matukio ya kihistoria kuhusu Joseph Smith na maandiko haya.

Maono ya Joseph Smith.

Katika 1820, Lucy Mack Smith aliamua kuungana na Kanisa la Kipresbiteria, na akawaambia watoto wake pia waungana naye. Wengine waliungana naye lakini wengine walikataa. Joseph Sr.alikataa kuungana nao. Mzee amekuwa akiwaambia familia yake kwamba Mungu amemtumia dini katika ndoto ambapo ilimanisha kwamba hakupaswa kwenda kanisani. Joseph Sr.aliishia kutojiunga na dini yoyote.

Siku moja katika muhula wa mwaka, Joseph Smith alikwenda kwenye mti jirani na nyumbani kwake na akamwomba Mungu amwambie ni kanisa lipi ajiunge nalo. Alidai kwamba Mungu Baba na Yesu Kristo walijitokeza kwake katika mwali wa moto ukiwa na mwanga kuliko mchana. Mungu alimwambia Joseph kutokuungana na makanisa yoyote kwa sababu yameharibika. Mungu pia akamwambia uwezo wake na mamlaka vilichukuliwa duniani katika karne ya kwanza A.D., na kwamba ingerejeshwa kwa muda mfupi.

Joseph hakumwambia mtu kuhusu ndoto hii hadi ilipofika 1838. Alijaribu kurudia kuhesabu toleo tofauti. Kwa mmoja kusema, kwa mfano, Mungu alimtokea na Yesu na baadhi ya malaika katika kitabu kingine kinasema: hakuna malaika.

Hatia ya Joseph Smith ya wizi.

Takriban miaka mitano hivi mnamo mwaka 1820, na labda miaka mingi baadae, Joseph Smith alijiingiza kwa sana katika uganga wa mizungu. Kutoka 1822, alipogundua “jiwe la utabiri” huko katika kisima cha Willard Chases, hadi 1827, alipotangaza “kutazama kwa kioo” katika makabiliano makubwa na baba mkwe wake, Isaac Hale, Smith alifahamika kwa uwezo wake wwa kutumia jiwe la kutabiri. Angeweza kuona vitu visivyo julikana , akiwashauri wachimba fedha katika sehemu iliyofukiwa hazina, machimbo yaliyojificha, n.k. Angeweza kulipwa kwa ajili ya huduma yake. Amewahi kujaribiwa na akapatikana na hatia ya wizi huu.

Smith alitaarifu kuwa usiku wa Septemba 21, 1823, malaika Moroni alishuka katika mnara mzuri wenye mwanga na kumwonyesha Smith jiwe iliyofukiwa huko hill Cumorah mwanzoni mwa karne ya hamsini. Ilishikilia kitabu cha maandiko yaliyoandikwa katika sahani ya dhahabu, kama ilivyotolewa na Mwokozi kwa wakazi wa zamani walioko katika bara la Amerika Kaskazini waliokuwa wana wa mkazi mmoja wa Kiyahudi aliyeongozwa pale na Mungu kutoka Yerusalemu kwenye mwaka wa 600 B.C. Sahani hiyo pia ilikuwa na Ngao ya jamii ya Kiyahudi, pamoja na Urim na Thummim – jiwe hilo ambalo lingempa Smith uwezo wa ajabu wa kusoma magombo ya zamani.

Mnamo Marchi 20, 1826, Joseph Smith Sr, alionekana mahakamani huko Bainbridge, New York. Alikuwa anashitakiwa kwa kuwa “mtu asiyekwenda kwa utaratibu au mwongo.” Hii ili maanisha ukosoaji wa ulaghai. Ndugu wa mkulima aliyejulikana kwa jina la Josiah Stoal(wakati mwingine ilitamkwa Stowell) akidai kwamba Smith alilipwa pesa baada ya kumshawishi Josiah mzee kwamba angeweza kupata fedha iliyofukiwa, machimbo ya chumvi, na vitu vingine vya thamani kwa uchawi.

Mwonekano wa mwenendo wa mahakama hiyo ilipelekea Smith kupatikana na hatia, lakini hakuna shitaka lilipelekea hukumu hiyo. Hitimisho iliyoenea ni kwamba haki ya amani iliyotolewa na Joseph kuondoka katika mji (kwa wakati ule ilijulikana kama “dhamana ya mguu”).

Wakati akimfanyia kazoo Stoal, Joseph na baba yake walihamia katika nyumba ya Isaac Hale huko Harmony, Pennsylvania. Wakiwa pale Joseph akakutana na binti wa Hale mrefu, na mwenye nywele nyeusi, aitwae Emma. Joseph na Emma walioana katika mji wa Zechariah Tarble wa Bainbridge Kusini, New York mnamo Januari 18:1827. Walilazimika kutoroka kutokana na baba yake na Emma kupinga ndoa hiyo. Wana ndoaa hawa wapya mara wakahamia katika mji wa Manchester kuishi na Joseph Sr.

Mwishoni Moroni akamwambia Joseph kuchukua sehemu ya sahani ya dhahabu na paraphernalia mnamo Septemba 22, 1827. Kwa kiwango fulani, neno limekuwepo katika mzunguko wa saham, kwa sababu katika siku iyo hiyo wanandoa walipopata tena sahani, wawinda hazina walilala macho wakizisubiri. Baada ya watu kushindwa kuonyesha vitu kutoka kwa Smiths, Joseph aliandika kwamba, bahati nzuri, alikuwa na mawazo mbadala ya kuficha sahani hizo katika tundu la kisiki wakiwa njiani kwenda nyumbani.

Willard Chase na dada yake, Sally, walingoza watu wengi wa mji katika juhudi tofauti kupigania sahani kutoka kwa Smiths. Walitoka bila kitu pamoja na kufanya majaribio mengi.

Hatika anguko, wanandoa wakakimbilia Harmony, Pennsylvania ili kuepuka mateso ya wasaka hazina. Walikusudia kuingia na Isaac Hale (Baba yake Emma), lakini Isaac alipoambiwa kuhusu "kitabu cha ajabu ya Sahani," kwa mashaka alihitaji kuziona. "Niliruhusiwa kusikia uzito wa box, na wakanipa kuelewa kwamba kitabu cha sahani kilikuwa kwenye – ambayo hataivyo, sikuruhusiwa kutazama."

Hii haikumridhisha baba yake na Emma, hivyo akaanzisha makatazo: aidha amuonyeshe yaliyoandikwa ndani ya kitabu, au ilizuiwa ndani ya nyumba. Kama suluhu ya mpito, Joseph alificha sahani kwenye miti. Majuma machache, Joseph na Emma wahamia katika nyumba yenye vyumba viwili ambayo ilikuwa ni ya kaka yake na Emma aitwaye Jesse, ambayo ilikuwa umbali wa mita 150 kutoka katika mji wa Isaac.

Tafsiri ya Joseph Smith.

Mara baada ya kuhamia katika nyumba ya Jesse, Joseph alileta box. Akitumia Urim na Thummim, alianza kutafsiri herufi zilizokuwa katika sahani ya dhahabu kwa Kiingereza. Kwa mawe ya ajabu, kitabu change cha concordance kinasema: "Kiebrania kwa neno hili inamanisha 'laana na ukamilifu.' Neno la Kiebrania 'Urim' inaanzia sentensi ya kwanza ya alfabeti ya Kiebrania (aleph) na 'Thummim' inaanzia sentensi ya mwisho (taw). Yalikuwa ni maneno matakatifu yaliyokuwa katika vifungu na zilitumika wakati wa vita ili kutazama mapenzi ya Mungu (angalia Hesabu 27:21). Imependekezwa kwamba ikiwa Urim ('laana') ilikuja baada ya kura kupigwa na jibu likawa 'hapana', lakini kama Thummim ('ukamilifu) inasema ilikuwa 'ndio.' Katika tukio lo lote, 'kila maamzi' yao ilikuwa 'kutoka kwa Bwana' (Mit. 16:33)."

Wakati Smith alipokuwa anatafsiri Kitabu cha Mormon, alihitaji pesa ya kulipia uchapishaji. Martin Harris, fanya vyema kwa ajili ya mkulima, aliandaliwa kwa ajili ya kuuza shamba lake kwa thamani $10,000 na ampe Smith hizo pesa ili alipie uchapishaji. Mkewe Harris Lucy aliyechukia. Ili kumtuliza na kurithisha shauku yake, Harris aliomba kuona sahani ya dhahabu. Badala yake Smith akataka kumwonyesha Harris nyaraka iliyoandikwa kwa mkono ya sehem ndogo ya sahani za dhahabu.

Harris alipeleka toleo la profesa Charles Anthon wa Chuo cha Colombia. Anthon alimwambia Harris kwamba alama zile zilikuwa za hazina lugha inayojulikana, na alihisi kwamba maelezo yote ya sahani za dhahabu ilikuwa ni uongo au utapeli. Harris akamwambia Smith, aliyejibu kwamba mfumo wa kuchimbua sahani za dhahabu ilikuwa ni ya muda mrefu na inayochosha, ambayo Wamomon (mwanzilishi wa andiko la zamani) aligeuza kuwa "mkono mfupi" alfabeti ya Kimisri kawaida haikujulikana kwa Anthon. Smith aliita "Mmisri aliyebadilika." Mara baada, ya kutoweka kwa kile kilichoitwa magombo ya Anthon.

Harris alimpa Smith $5,000 kuchapisha nakala 3,000, kwa nia ya faida. Baadae Harris akafanya kazi kama mwandishi wa Smith, akiandika maneno matakatifu Smith akiwa anayaongea nyuma ya blangeti uliotanda katika chumba. Karibia miezi miwili hivi watu hawa wakatengeneza "Kitabu cha Lehi," wakijumuisha ukrasaa 116 kutoka kwa sahani za Mormon.

Kumwongoa mkewe, Harris alipeleka kurasa 116 kwa Palmyra ili amwonyeshe. Alirudia kwa Harmony majuma machache akilia na kufadhaika. Alimwambia Joseph kwamba kurasa zimepotea nyumbani kwake na zisingeweza kukusanywa.

Ni lazima Joseph Smith alihitimisha kwamba Lucy Harris alichana kurasa 116 ili kwamba ashushe hadhi kazi ya uchapishaji. Kama na alipotafsiri Kitabu cha Lehi ilikataa kufanana na kurasa ambazo Lucy alishikilia kuwa mbadala wa sehemu nyingine, uhaalali wa kazi mpya ungeharibika.

Hivyo, Joseph hakutafsiri sehemu ya sahani ya dhahabu. Alieleza kwamba Mungu alichukizwa kwamba Smith alimruhusu Harris achukue tafsiri ya kwanza aliyokuwa ameondoa Urim na Thummim. Baadae Mungu akarudisha jiwe la mwonaji kwa Smith lakini akamwagiza asitafsiri kitu ambacho tayari kilikuwa kimepotea. Hivyo, Kitabu cha Mormoni kunaanzia Kitabu cha Nephi na siyo na Lehi.

Kwa kweli, Smith aliendelea na tafsiri yake ya Kitabu cha Mormon akianzia pale alipoishi, akirudi nyuma kutengeneza sehemu ya historia ya kale (Toleo ya Nephi) baada kila kitu kukamilishwa.

Smith na Cowdery walianzia kazi magombo na wakamaliza maneno 275,000 ya magombo mapema Juli ya 1829. Walipaswa kuwa na kiwa cha takribani maneno 3,700 kwa siku.

Joseph Smith alieleza kwamba sahani zilichukuliwa na malaika. Hivyo, hazipatikani kwa kuchunguzwa na kukadiriwa.

Tafsiri ya Joseph Smith ya maneno ya kimisri.

Mnamo Julai ya 1835, mtu mmoja kutoka Ireland aitwaye Michael Chandler alileta uthibitisho ya mummies w Kimisri na papyri hadi Kirtland Ohio, hadi nyumbani kwa Wamormoni gombo lilikuwa na maandishi ya Kimisri. Mnamo 1835 maandishi hayo yalikuwa hayasomeki.

Kama Nabii na mtu wa maajabu wa Kanisa, Joseph Smith alipewa amri ya kutazama katika maandishi ya kwenye magombo katika kuthibitisha na kwa mushtuko wa kila mmoja, ilifunuliwa kwamba 'gombo moja lilikuwa na maandishi ya Abraham, nyingine maandishi ya Joseph wa Misri" (Historia ya Kanisa, Tol.2:236. Juli 1835). Kanisa lilinunua vithibitosho kwa $2,400. Joseph alimaliza tafsiri ya kitabu cha Abraham baadae kidogo, lakini kitabu cha Joseph haikutafsiriwa. Gombo lilipotea mara baada na ikafikiriwa kwamba imeteketezwa huko Chicago mnamo 1871. Hivyo, basi kulikuwa hakuna namna ya kuhuisha tafsiri ya Joseph. Kama gombo lingeonekana na kutafsiriwa ingeweza kuthibitisha au kutothibitisha uwezo wa Joseph kama

nabii wa Mungu. Baada ya yote alipaswa kuwa nabii na kuwa na uwezo wa nguvu za giza wa kitabu cha Mormon na kitabu cha Abraham yawezekana ilithibitisha.

Mnamo Oktoba ya 1880 Lulu yenye thamani, mchanganyiko wa maandishi, ilikuwa na kitabu cha Abraham, ilitambulika kama andiko na Kanisa la Mormon.

Kwa mshangao wa kila mmoja, mnamo 1966 gombo liligundulikwa katika moja ya vyumba vya kumbukumbu vya uchoraji. Taarifa ya mji we bahari ya chumvi mnamo Nov. 27, 1967 akakubali ugunduzi wa gombo. Nyuma gombo kulikuwa na na "michoro ya hekalu na ramani za Kirtland, mtaa wa Ohio." Hakupaswi kuwa na shaka kwamba hii ndio ilikuwa waraka sahihi ambayo Joseph Smith aalitafsiri kitabu cha Abraham.

Kwa gombo kugunduliwa na mwandishi wa Kimisri tangu miaka ya 1800, hivyo ingekuwa kazi rahisi ya kutafsiri gombo na kuthibitisha mara moja kwa yote kwamba Joseph Smith alikuwa ni nabii kwa zawadi yaa "jiwe la ajabu" wakati ni madai yaliyotolewa na kanisa la Mormon. Hii ingeweza kuthibitisha ukweli wa kitabu cha Mormon na kitabu cha Abraham na vingeweza kumthibitisha Joseph Smith kama nabii wa kweli wa Mungu.

Wazoefu wanasemaje? Joseph Smith aalichukua michoro mitaatu kutoka katika magombo ya Misri, na akazipa majina kama Facsimile No1, Na. 2, na Na. 3, na akazishirikisha na kitabu cha Abraham kwa maelezo ya nini zilikuwa. Mwana logists wa Kimisri ameitazama michoro naa kupata tafsiri ya Joseph Smith kuwa ilikosewa. Lakini Wamormon, katika kujitetea katika kitaabu kitakatifu walisemaa kwamba Facsimile pekee haikutosha kuonyosha kwamba Joseph Smith alikuwa anakosea katikaa uwezo wake wa kutafsiri. Kwa ugunduzi wa gombo, siyo kwamba hakukua na michoro inayofanana katika gombo, na ndivyo ilivyo andiko ambamo Joseph Smith alifanya tafsiri yake. Sasa ilikuwa inawezekana kudhihirisha usahihi wa uwezo wa kutafsiri wa Smith.

Facsimile No.1

Joseph Smith alisema kuwa Facsile Na 1 ilikuwa mbaya kama "malaika wa Bwana" pamoja na "Abraham kufunga kwenye hema", "ikiwa imetolewa dhabihu na kuhani asieyefaa." Vyungu vilivyo chini ya hema vilikuwa ni miungu tofauti "Elkenah, Libnah, Mahmackrah, Korash, Pharaoh," n.k. Kwa uhalisia, "tukio linaloonyesha ugonjwa umelala kooni mwa simba."

Kwenye kombo la awali, mchoro huu umeshikishwa kwenye hieroglyphic ambamo Joseph alitohoa mwanzo wa kitabu cha Abraham ambayo inaanza na maneno, "Katika nchi ya Wakaldayo, katika makazi ya baba, Mi, Abraham, niliona kwamba inafaa kwangu mimi kuwa na sehemu ya makazi"(1:1). Kwa uhalisia, hieroglyphics inaitafrisi kama, "Osiris itaonyeshwa katika bwawa la Khons – na pia kwa Osoris Hor, imedhihirishwa, amezaliwa Tikhebyt, amedhihirishwa – baada ya mkono wake kuwekwa katika roho na kupumua kunaruhusu (ambayo [Isis] imetengenezwa na inamaandishi pembeni na nje) imefungwa kwenye nguo nzuri ya kifaalme na kuwekwa katika mkono wake wa kushoto karibu na moyo wake;vifaa vingine

vimeifunga kwa kuizunguka. Mtu ambaye kitabu kiliharirwa kwa ajili yake atapumua milele kama sauti za miungu zinavyofanya.” Haya yalikuwa ni maelezo ya jinsi ya kuhifadhi na kufunga mwili uliokufa. Nakala yote ilitafsiriwa vibaya, alafu bado Wamormon wanachukulia tafsiri hizi kuwa za kweli.

Joseph Smith – nabii wa uongo.

Tukitazama nyuma, ni wazi kuamini kwamba Joseph Smith hakufanya tafsiri mzuri wa kitabu cha Abraham. Wakati, mnamo 1967, gombo lililinganishwa, maakosa yake ya kutafsiri kutoka sehemu moja na kulinganishwa na nyuma E. Smith alitafsiri kitabu hiki kimoja katika maneno 76, na majina tisa ya msingi na majina. Tabia ya mungu wa Misri Khonsu ilitafsiriwa na Smith katika maneno 177 katika Abraham 1:16-19.

Inapaswa kuwa wazi kwamba wanafunzi wa sasa wamegundua kwamba Josepha Smith hakutaafssiri kitabu cha Abraham kwa uwezo wa Mungu kama alivyodai. Inafuatia kwamba kama hakutafsiri kitabu cha Abraham kwa uwezo wa Mungu, na hivyo hakuweza kufanya hivyo hata kwa kitabu cha Mormon.

Kwa mara ya kwanzaa Joseph alipotoa tafsiri yake ya kwanza, hizi hieroglyphic zilikuwa hazina mipangilio. Leo ni ugunduzi wa “Jiwe la Rosetta.” Alikuwa salama kusema chochote alichotaka na hakukuwa na njia yoyote ya kuthibitisha uongo wake. Lakini kwa kubadilisha gombo ilo hilo alilotumia katika tafsiri ya kitabu chake cha Abraham, na ukweli kwamba hakuifanya vizuri kwa usahihi, inaweza ikawa kithibitisho tosha kwamba Joseph Smith alisema uongo kuhusu uwezo wake kutoka kwa Mungu. Ameonyeshwa kuwa nabii muongo.

Kuna vitu vingine vingi katika maisha ya Joseph Smith yanayoonyeshaa alikuwa nabii wa uongo naa mtu mwovu. Kuna rekodi ya maisha ya mashtaka ambayo bado inaishi leo.

Benki Isiyo halali.

Alianzisha benki isiyo halali (Mungu alimwambia kuanzishaa, lakini uongozi wa jiji haikumpa jina). Lakini alianzisha nyingine. Ili kuwavutia wawekaji pesa, alijaza maboksi kadhaa kwa mchanga, mfuniko wa chuma, na mawe, alafu akazifunika kwa sarafu ya shilingi hamsini. Wateja waliovutiwa walikuwa wanaingizwa katika sehemu zilizokuwa zile boksi na kuonyeshwa sarafu zilivyojaa. Maana wawekezaji wa mwezi ujao wangekuja kama nyuki kwa asali. Alitumia pesa zile kununu mashamba katika ya mji na shamba lenye hekari 140. Sheria ilionyessha nyaraka dhidi ya benki, na watu walidai warudishiwe pesa zao, na ilibidi atoroke kuhofia maisha yake, akiacha madeni makubwa.

Wakati alipokuwa akiwapiga washirika kwa ajili ya dini yake, na magazeti ya mjini yangeandika kitu chochote juu yake, angeweza kuharibu machapisho yao.

Joseph Smith na Wamarekani wa Kihindi.

Madai ya Smith kwamba Wamarekani wa Kihindi ilikuwa ni uzao wa Kiyahudi waliokuja Marekani mnamo 600 B.C ni wajinga. Wanaekolojia wanasema hakuna ushahidi juu ya hili, hataivyo kuna ushahidi kinyume. Mifumo ya mfupa ya Wamarekani wa Kihindi haikuwa kama ile ya Kiyahudi, bali ya wale walioko Mashariki mwa Asia.

Wazo la kwamba Yesu Kristo aliwatembelea Wamarekani wa Kihindi na akawapa dini ya Ukristo kama ilivyotengenezwa kaatika kitabu cha Mormon pia ni ujinga. Dini yao kama ilivyoonyeshwa katika rekodi ya akaeolojia mara zote imekuwa ni ibadaa ya wanyama, jua, mwezi, n.k.

Manabii wa Joseph Smith walimkana.

Wawili kati ya mitume wake wa mwanzo na mashahidi walimkana Joseph Smith kama mwongo kabla hawajafa. Oliver Cowdery na Martin Harris walikuwa mashahidi wake wakuu kuhusiana na sahani za dhahabu. Joseph Smith alimuita Harris mwanadamu "pia kumanisha kuonyesha; mtu mwovu"; Cowdery alikataa Umormon na kuungana na kanisa la Wamethodist. Shahidi wa tatu, David Whitmer, alimuita Smith nabii aliyeanguka.

Martin Harris, mwongofu wa kwanza wa Umormon nje ya familia ya Joseph, shauri la ukweli uwezo wa somo la kidini. Wakati wa uhai wake, alibadilisha mfumo wa kidini mara kumi na mbili au kumi na tatu, ukijumulisha kubadilishana katika imani hata baada ya kuwa mfuasi wa Joseph Smith. Kwa wakati mmoja, baada ya kuondolewa katika Kanisa, akawa mfuasi wa Anna Lee, muanzilishi wa kundi linalojulikana kama Shakers. Phineas Young, ndugu wa nabii ajaye Brigham Young, alieleza kwamba Martin Harris alidai kwamba ushuhuda wake kwa imani ya Shaker ilikuwa na nguvu kuliko ushahidi wa kitabu cha Mormon.

Ushahidi unaoharibu kitabu cha ushahidi wa Mormon unatoka kwa Martin Harris. Katika barua ya Mwongofu wa awali wa Mormon, Stephen Burnett, anaeleza ni kwa nini aliamua kuachana na Kanisa: "…lakini niliposikia Martin Harris akieleza hadharani kwamba hakuwahi kuiona sahani kwa macho yake ya assili isipokuwa kwa ndoto na fikra, siyo Oliver au Daudi & pia kwamba shahidi wa nane hakuziona & akawa na shaka kutia sahihi chombo hicho kwa sababu hiyo, lakini tumeshaawishiwa kuifanya, jaribio la mwisho likatoa nafasi…hivyo mimi majuma matatu niko katika jiwe la asubuhi…sababu iliyopelekea nichukue hatua amb ayo nilikatazwa kufanya na kukubali kitabu cha Mormon."

Mitume watatu pia waliacha kanisa la Mormon.

Unabii mwingine wa uongo zaidi.

Josepha Smith alifanya unabii ambao haukuwahi kutimizwa, kama vile "vita itamwagwa kwa mataifa yote kwanzia Carolina Kusini, na kwamba kutakuwa na njaa, mapigo, tetemeko la ardhi, na …mwisho wa mataifa."

Kumb. 18:22, "*Atakaponena nabii kwa jina la BWANA, lisifuate jambo lile wala kutimia, hilo ndilo neno asilolinena BWANA; kwa kujikinai amelinena huyo nabii, usimwogope.*"

Wamormon wanaamini nini naa Biblia inasema nini?

Kwamba kuna miungu mingi.

Joseph Smith, "Ninapenda kutangaza kama ilivyo kila siku na katika makusanyiko yote ambapo nimehubiri juu ya somo la Uunga, imekuwa ni wingi wa miungu." (Historia ya kanisa 6:474).

Brigham Young, rais wa pili na nabii wa kanisa la Mormon, kuna miungu mingapi, sijui. Lakini hakukua na wakati ambapo hakukua na miungu…" (Journal of Discourses 7:333).

- Kumb. 4:35, "*Wewe umeonyeshwa haya ili upate kujua ya kuwa BWANA ndiye Mungu hapana mwingine ila yeye.*"
- Isa. 44:8, "*Msiogope wala msifanye hofu; je! Sikukuhubiri haya zamani na kuyaonyesha? Na ninyi ni mashahidi wangu. Je! Yuko Mungu zaidi yangu mimi? Hakika hapana Mwamba mimi sijui mwingine.*"
- 1 Kor. 8:4, "*Basi kwa habari ya kuvila vitu vilitolewa sadaka kwa sanamu; twajua ya kuwa sanamu si kitu katika ulimwengu, na ya kuwa hakuna Mungu ila mmoja tu.*"

Kwamba Mungu Elohim ni sawa na Adam na Baba wa Kristo, na kwamba alikuwa mwanadamu kama tulivyo.

Orson Hyde, "Mungu Baba yetu wa Mbinguni labda wakati fulani alikuwa mtoto na wa kawaida kama tulivyo, na akaibukia hatua kwa hatua katika mfumo wa ukuaji, katika shule ya viwango vya juu; ameendelea mbele na kushinda, hadi alipofikia hatua ambapo sasa ni."(Journal of Discourses 1:132).

"…baba yetu wa mbinguni wakati fulani alikuwa mwanadamu kama tulivyo, akiwa na uwezo wa kufa kimwili." (Achieving a Celestial Marriage, uk.132).

- Zab. 90:2, "*Kabla haijazaliwa milima wala hujaiumba dunia, na tangu milele hata milele ndiwe Mungu.*"
- Zab. 93:2, "*Kiti chako kimekuwa thabiti tokea zamani; wewe ndiwe uliye tangu milele.*"

Kwamba mwanadamu naa miungu ni sawa.

John Widtsoe, "Mungu na wanadamu ni viumbe sawa, wanatofautiana tu katika uweza wao wa kufikiri." (Gospel Through the Ages, uk. 107).

Joseph Smith, "Mungu mwenyewe pia alikuwa kama tulivyosisi, na ni mwanadamu anayeinuliwa, na anakaa kiti cha enzi mbinguni." (Teachings of the Prophet Joseph Smith, uk. 345).

Milton Hunter, “Hakuna na rekodi aliyetoa maelezo yanayojitosheleza ya mafundisho yanayoonyesha kwamba mwanadamu anaweza kuwa Miungu kama alivyofanya nabii wa Kimarekani, Josepha Smith.” (Gospel Through the Ages, uk.115).

- Isa. 43:10, “*Ninyi ni mashahidi wangu asema BWANA, na mtumishi niliyemchagua; mpate kujua na kuniamini, na kufahamu ya kuwa mimi ndiye; kabla yangu hakuumbwa Mungu awaye yote wala baada yangu hatakuwepo mwingine.*”
- Ufu. 21:3, “*Nikasikia sauti kubwa kutoka katika kile kiti cha enzi ikisema, tazama maskani ya Mungu ni pamoja na wanadamu, naye atafanya maskani yake pamoja nao, nao watakuwa watu wake. Naye Mungu mwenyewe atakuwa pamoja nao.*”

Kwamba mwanadamu kama Miungu mbinguni atakuwa na wanawake na kuzaa watoto.

Brigham Young, “Katika ufufuo, wanadamu ambao wamekuwa waaminifu na wenye juhudi katika mambo yote yahusuyo mwili …na (wana) wanafaa kutunikiwa na Miungu, …watateuliwa kusimamia mambo, hiyo ni, kuwa waumbaji kwa haki yao wenyewe. Kuliko kuwa na uwezo wa kuzaa watoto kimwili, sasa wanaweza kuzaa watoto wa kiroho.

Orson Prat, “Ni nani atakayekuwa somo katika ufalme ambao watauongoza…? Watoto wao wenyewe, mafanikio yao binaafsi itakuwaa taifa la falme zao; kwa maneno mengine, mfumo wa mababu utatawala pale bila kuwa na mwisho wa milele, na watoto wa kila mzee atakuwa wake wakati nyakati za milele ukiendelea.” (Journal of Discourses, 15:319).

- Mat. 22:30, “*Kwa maana katika kiyama hawaoi wala hawaolewi, bali huwa kama malaika mbinguni.*”

Kwamba Joseph Smith alifundisha kwamba wingi wa wanawake ulikuwa mpango wa Mungu.

Mnamo Julai 12, 1843, Joseph Smith alidai kupokea ufunuo kwamba wanaume walipaswa kuwa na wanawake wengi na masuria na kuitangaza “agano jipya na la mwisho.” (Doctrine and Covenants, 132:1,4).

Waale walioikataa waliangamizwa. Inaonekana kwamba mkewe wa kwanza aliwapinga wanawake wapya amabo mumeo alikuwa anawaleta na masuria nyumbani kwake; hivyo akapokea maono maalum kwa ajili ya mkewe: “na mfaanya kazi wangu, Emma Smith, awapokee wale wote waliotolewa kwa mtumishi wangu Joseph … Lakini kama hatakubali agizo hili ataangamizwa, asema Bwana.” (Doctrine and Covenants 132:51-56). Ingekuwa vigumu kuwa na mwanaume anayewatamani wanawake wengine na akadai kuwa ni msemaji wa Mungu.

Brigham Young alikuwa na wake 17 naa watoto 56. John Lee alikuwa na wake 19 na watoto 64.

Wamormon wanafundisha kwamba Yesu alikuwa na wake wawili, Mariamu na Martha, na alikuwa na watoto nao. Hataivyo, Bibilia haisemi kitu kama hicho.

Orson Hyde, “Itazaliwa akilini kwamba wakati fulani, kwamba kulikuwa na ndoa huko Kana ya Galilaya; na katika usomaji makiji wa ubadilishaji huo, itagundulika kwamba hakuna mtu yeyote isipokuwa Yesu Kristo aliyeowa siku ya tukio hilo. Kama hakuoa, uandani wake na Mariam pamoja na Martha, na yule Mariam mwingine ambaye Yesu alimpenda zaidi, isingeweza kusemwa vizuri kwa hali ya juu na sio vyema kuiongelea.” (Journal of Discourses, Tol. 4, uk.259).

Hitimisho la Hyde linashindwa kwa sababu rahisi kwamba Yesu alikaribishwa kwenye harusi huko Kana. Yoh. 2:1-2, “Na siku ya tatu kulikuwa na harusi Kana ya Galilayaa; na mama yake Yesu alikuwepo: Na Yesu na mitume wake wote waliitwa kusherekea harusi.” Kama kweli alikuwa ni bwana harusi, mwaliko kama huo haukuwa na maana.

Sheria za Marekani zilikataza kuwa na wanawake wengi mnamo 1871. 1890, rais wa Mormon Wilford Woodruff rasmi akakataza watu kuoa wanawake wengi kama tendo la kanisa la Mormon, haijalishi Joseph Smith angesema nini juu ya hili “an eternal covenant.”

Matt. 19:9, “*Nami nawaambia ninyi kila mtu atakayemwacha mkewe isipokuwa kwa sababu ya uasherati, akaoa mwingine azini; naye amwoaye yule aliyeachwa azini.*

Efe. 5:31, “*Kwa sababu hiyo mtu atamwacha baaba yake na mama yake, ataambatana na mkewe na hao wawili watakuwa mwili mmoja.*”

Kutazama meza ya Bwana.

1 Kor. 11:23-29, “*Kwa maanaa mimi nalipokea kwa Bwana niliyowapa ninyi, ya kuwa Bwana Yesu usiku ule aliotolewa alitwaa mkate, naye aakiisha kushukuru akaumega akasema huu ndio mwili wangu ulio kwa ajili yenu; fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu. Na vivi hivi baada ya kula akakitwaa kikombe akisema kikombe hiki ni agano jipya katika damu yangu; fanyeni hivi kila mnywapo kwa ukumbusho wangu. Maana kila mwulapo mkate huu na kukinywea kikombe hiki, mwaitangaza mauti ya Bwana hata ajapo. Basi kila alaye mkate huo, au kukinywea kikombe hicho cha Bwana isivyostahili, atakuwa amejipatia hatia yaa mwili na daamu ya Bwana. lakini mtu ajihoji mwenyewe, na hivyo aule mkate naa kukinywea kikombe. Maaana alaye na kunywa, hula na kunywa hukumu yaa nafsi yake kwa kutokuupambanua ule mwili.*”

Baada ya kurudia kwa kaarne, kanisa la Mormomon likabadilisha matendo yao kutoka katika matumizi ya mvinyo katika meza ya Bwana wakaanza kutumia maji, kwa sababu walidhani mvinyo unatokana na shetani. Hii inaendana na fikra zao kwamba kahawa na chai ni mbaya kunywa.

Kuwa makini na Umormon wanapotoa mashambulizi dhidi ya Biblia.

Ni vigumu kujadiliana na Wamormon wanaotoa huduma chache kwa Biblia katika kipeperushi chao cha nane cha imani, “Kwanza Biblia ni Neno la Mungu kama ilivyotafsiriwa sahihi”, lakini kiualisia hawana ujasiri nao kwa sababu ya matatizo haya:

- Ina matatizo ya utafsiri (ikiandika matatizo chini katika karne zote).
- Inamkanganyiko na makosa.
- Haina vitabu vingine naa mafundisho.
- Ni sehemu pekee ya ufunuo wa Mungu kwetu.
- Haiku waazi na ni vigumu kuitafsiri vizuri. Swala laa tafsiri, au kuamisha.

Kuna vipengele vingi duniani kote (lugha zingine pamoja na Kiebrania na Kiyunani) kwa nyakati tofauti ikilinganishwa inaonyesha kwamba Mungu amelitunza neno lake, kama alivyosema atalitunza.

- Zab. 12:6-7, “*Hema za wapokonyi hufanikiwa, na hao wamkasirishao Mungu hukaa salama; mikononi mwao Mungu huleta vitu vingi. Lakini sasa waulize hao wanyama, nao watakufundisha; na nyuni wa angani nao watakuambia;*”
- 1 Pet. 1:23-25, “*Kwa kuwa mmezaliwa mara ya pili; si kwa mbegu iharibikayo bali kwa ile isiyoharibika; kwa neno la Mungu lenye uzima, lidumulo hata milele. Maana mwili wote ni kaama majani, na fahari yake yote ni kama ua la majani. Majani hukauka na ua lake huanguka; bali neno la Bwana hudumu hata milele. Na neno hilo ni neno lile jema lililohubiriwa kwenu.*”
- Mat. 5:18, “*Kwa maana amini nawaambia, mpaka mbingu na nchi zitakapoondoka, yodi moja wala nukta moja ya torati haitaondoka, hataa yote yatimie.*”
- Mat. 24:35, “*Mbingu na nchi zitapita lakini neno langu halitapita kamwe.*”

Mkanganyiko.

Ulimwengu umedhani kwamba wamepata mkanganyiko kwenye Biblia, lakini kwa wanafunzi wa Biblia mara nyingi zinaelezwa kirahisi.

Haaina vitabu vingine na mafundisho na ni sehemu tu ya ufunuo wa Mungu kwetu.

Kuna sehemu zingine kwenye Biblia ambazo zinaongelea mambo mengine yaliyoandikwa ambazo hatuna, kama maandishi ya Paulo kwa baadhi ya makusanyiko, lakini kuondoa kwake hakumanishi kwamba hatuna sehemu ya mpaango wa Mungu. Inaweza ikawa ni vitu ambavyo vimeshaongolewa sehemu nyingine.

- 2 Tim. 3:16-17, “*Kila andiko lenye pumzi ya Mungu lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza na kwaa kuwaadibisha katika haki; ili mtu wa Mungu awe kamili amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema.*”
- 2 Pet. 1:3, “*Kwa kuwa uweza wake wa Uungu umetukirimia vitu vyote vipasavyo uzima na utauwa, kwa kumjua yeye aliyetuita kwa utukufu wake na wema wake mwenyewe.*”

- Yuda 1:3, "*Wapenzi nilipokuwa nikifanya bidii sana kuwaandikia habari ya wokovu ambao ni wetu sisi sote, naliona imenilazimu kuwaandikia ili niwaonye kwamba mwishindanie imani waliokabidhiwa watakatifu mara moja tu.*"

Haiku wazi na ni vigumu kuitafsiri vyema.

Kama kuna kifungu ambayo tunaona ni ngumu, kuna vyanzo vingi vinavyoweza kutusaidia: kamusi, lexicon, concordance, n.k. hakuna mbadaalaa mzuri wa ujuzi kuliko kuwa na ujuzi ambao Mungu anataka tuwe nao katika kusomaa neno lake. Kwa bahati mbaya, watu wengi wanashindwa kufanya hili katika maisha yao.

Hataivyo, kitabu cha Mormomon kimeboreshwa miaka mingi kujaribu kurudiaa maneno ambayo inawapendezaa wao. Ninacho kitaabu kinachoonyesha maatoleo ya zamani nay a sasa ikionyesha mabadiliko yao yote.

Hitimisho

Joseph Smith anadai kupokea maagizo kutoka kwa malaika wa Mungu. Hata kama kile anachosema kilitokea, Mungu anasemaje kuhusu kupokea ujumbe kama huo kutoka kwake?

- 1 Yoh. 4:1, "*Wapenzi msiamini kila roho, bali zijaribuni hizo roho, kwamba zimetokana na Mungu; kwa sababu manabii wa uongo wengi wametokea duniani.*"

Gal. 1:8-12, "*Lakini ijapokuwa sisi au malaika wa mbinguni atawahubiri ninyi injili yoyote isipokuwa hiyo tuliyowahubiri, na alaaniwe. Kama tulivyotaangulia kusema, na sasa nasema tena, mtu awaye yote akiwahubiri ninyi injili yo yote isipokuwa hiyo mlioipokea na alaaniwe. Maana sasa je! Ni wanadamu ninaowashawishi au Mungu? Au nataka kuwapendeza wanadamu? Kama ningekuwa hata sasa nawapendeza wanadamu, singekuwa mtumwa wa Kristo. Kwa maana ndugu zangu injili hiyo niliyowahubiri, nawajulisha ya kuwa siyo ya namna ya kibinadamu. Kwa kuwa sikuipokea kwa wanadamu wala sikufundishwa na mwanadamu, bali kwa ufunuo wa Yesu Kristo.*"